**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022


**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. DKT. SOUD NAHODA HASSAN**
**WAZIRI, WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**


**MEI, 2021**



**MHE. DKT. SOUD NAHODA HASSAN**
**WAZIRI, WIZARA YA KILIMO,**
**UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**

# YALIYOMO

UTANGULIZI ............................................................. 1
MIONGOZO YA MHE. RAIS DKT. HUSSEIN ALI MWINYI KATIKA KULETA MAGEUZI YA SEKTA YA KILIMO ............................................................. 4
UKUAJI WA SEKTA YA KILIMO NA UZALISHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ............................................................. 5
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021 ............................................................. 7
MUUNDO WA WIZARA NA UTEKELEZAJI (2020/2021) . 8
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021 ............................................................. 9
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2020/2021 ............................................................. 11
CHANGAMOTO............................................................. 17
HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO............................................................. 17
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA 2020/2021 ............................................................. 19
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO............ 19
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji..................... 20
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ..................................... 22
Programu Ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula ............. 24
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ............................................................. 26
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU............................................................. 26
Programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu........... 27
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO........... 28
Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo........... 29

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar....................................30
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAZI
ZA WIZARA YA KILIMO. ....................................................31
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji............................32
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti .........................33
Programu Ndogo ya Uratibu naUtekelezaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili na Mifugo Pemba .......................................34
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ...........................................................35
MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022. ...................................................36
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO.......................38
Programu Ndogo ya Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji ...............................................................39
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. ..........................................................40
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..........................................................................41
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI........................41
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU..............................................................................42
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO...........43
Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo...........44
Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI......................................45
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO ..................................................................45
Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji..............................46
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti .........................46
Programu Ndogo ya Uratibu Kazi za Kilimo, Umwagiliaji,

Maliasili na Mifugo Pemba.....................................................47
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ..........48
SHUKURANI.............................................................................49
VIAMBATISHO ........................................................................51

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa Fedha wa 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima wa afya na kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Ni dhahiri kwamba amani na utulivu umezidi kuimarika kwa kuendelea kwa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Nane ya Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Umahiri na uadilifu katika uongozi wake umekubalika hapa Zanzibar na tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, maarifa na hekima zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu na kuleta maendeleo makubwa.

3. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025; kwa kuimarisha utawala bora, demokrasia na hasa mapambano dhidi ya rushwa, adui maradhi, njaa na umasikini kwa mafanikio makubwa. Mafanikio hayo yameanza kubadilisha na kuleta mageuzi ya uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya mapato, jambo

ambalo linawavutia wawekezaji, na imepelekea Serikali za nchi zilizoendelea na wahisani kuwa na imani na Serikali na hivyo kuwavutia katika uwekezaji na kuwafanya waendelee kutoa misaada katika sekta za kiuchumi na kijamii.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena nazipongeza pia juhudi za Mheshimiwa Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali kupitia maagizo, maelekezo, ziara zake na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji wa Serikali. Hatua hizo zimeweza kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa majukumu ya Wizara na taasisi za Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa kwanza Mwanamke katika historia ya Tanzania na kwa Afrika ya Mashariki. Aidha, tunamuombea dua kwa Mwenyezi Mungu ampe nguvu, uwezo na maarifa ya kuliongoza Taifa hili ili liendelee kuimarika kiuchumi na kufikia malengo yanayokusudiwa.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT Wazalendo. Vilevile, nampongeza pia Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa juhudi zao kubwa za kumsaidia na kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi kwa kuleta maendeleo na ustawi wa jamii.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi kwanza kwa kuchaguliwa kwa kishindo na kupata kura zote za ndio wakati wa kugombea nafasi hiyo, uzoefu na umahiri wako umepelekea kuliongoza vizuri na kwa ufanisi Baraza hili Tukufu ambalo linatoa maamuzi mazito katika kusimamia demokrasia, utawala bora na maendeleo ya nchi yetu.

8. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo, Biashara na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir, Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufuatilia utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 pamoja na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022 wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara hii. Napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

9. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Paje kwa kuendelea kunipa mashirikiano na kuwa na imani na mimi katika kusimamia na kuleta maendeleo ya jimbo hili. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni. Aidha, napenda kuishukuru familia yangu kwa kunipa ushirikiano na kuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa katika majukumu ya kitaifa.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa napenda kutoa pole kwa Taifa letu la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na viongozi wetu wakuu wapendwa

akiwemo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliekuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya tano na Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad aliekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar wa awamu ya nane. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Vilevile, tunamuomba Mwenye Enzi Mungu mwingi wa rehma atupe shufaa na ayaondoshe maradhi haya ya CORONA nchini mwetu na duniani kote - AMIN.

## MIONGOZO YA MHE. RAIS DKT. HUSSEIN ALI MWINYI KATIKA KULETA MAGEUZI YA SEKTA YA KILIMO

11. **Mheshimiwa Spika,** katika awamu hii ya Nane, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo itaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Saba katika kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza kwa mahitaji ya chakula kama ilivyoelezwa na Mhe Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa Ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi ambapo alisisitiza kuendeleza kilimo biashara na chenye tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha umwagiliaji pamoja na ujenzi wa vitalu nyumba (green houses) na matumizi ya zana za kilimo, pembejeo na mbegu bora.

12. **Mheshimiwa Spika,** Juhudi nyengine zitakazochukuliwa na Wizara ya Kilimo katika Serikali hii ya Awamu ya Nane katika kukuza uchumi wa Zanzibar ni pamoja na kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda, mazao ya mizizi na miwa ambayo ndio chachu ya maendeleo katika sekta ya viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la Nazi na Karafuu nchini. Vilevile Wizara ya Kilimo itaendelea na

utoaji wa miche ya mikarafuu na minazi kwa wakulima bila ya malipo. Aidha, Wizara itahakikisha upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji wenye tija na matumizi ya mbegu bora za mifugo.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Maliasili, Wizara ya Kilimo inaendelea na usimamizi wa maeneo ya misitu ya hifadhi na ya jamii kwa lengo la kuhifadhi bioanuai, mazingira pamoja na kuimarisha huduma za utalii. Wizara pia itaendeleza kampeni za upandaji miti kitaifa katika maeneo yenye vyanzo vya maji, mashamba ya Serikali, maeneo ya wazi pamoja na kushajiisha wananchi kupanda miti ya matunda na misitu katika mashamba yao kwa kuhifadhi mazingira, kuweka haiba nzuri ya nchi yetu na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

## UKUAJI WA SEKTA YA KILIMO NA UZALISHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

14. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za mazao, mifugo na misitu inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar na inatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha pamoja na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora. Kwa mwaka wa fedha 2020 Sekta ya Kilimo imechangia kwa asilimia 27.6 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 21.2 kwa mwaka 2019 (OCGS 2020). Aidha, Sekta hii inaendelea kutoa ajira rasmi kwa wastani wa asilimia 45 kwa wakaazi wa Zanzibar na hivyo ina mchango mkubwa katika ustawi wa jamii.

15. **Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Wizara ni kuimarisha utendaji na usimamizi wa sekta kwa kuongeza wigo wa

mapato, uzalishaji kibiashara na wenye tija kwa mazao ya chakula, biashara na mifugo kwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, utiaji wa thamani, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza viwanda na pato la Taifa .Aidha, Wizara pia inasimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili za misitu na kuendeleza utalii.

16. **Mheshimiwa Spika;** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula, matunda na mboga umeongezeka; ikiwemo ndizi zimeongezeka kutoka tani 65,321 mwaka (2019) hadi tani 66,840 (2020) sawa na asilimia 2, viazi vitamu tani 53,996 (2019) hadi tani 57,284 (2020) sawa na asilimia 6, mahindi tani 1,600 (2019) hadi tani 1,907 (2020), sawa na asilimia 19 na uzalishaji wa mboga na matunda umeongezeka kutoka tani 43,080 (2019) hadi tani 54,935 (2020) sawa na asilimia 28. **(Kiambatanisho Nam. 1A)**. Hali hii imetokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa, muamko wa wakulima katika kuendeleza kilimo, matumizi ya teknolojia za uzalishaji na pembejeo pamoja na kuongezeka kwa ekari zilizopandwa kufikia 100,907 mwaka 2020 kutoka ekari 97,577 mwaka 2019 sawa na asilimia 2.7 **(Kiambatanisho Nam. 1B)**

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, takwimu zinatuonesha uzalishaji wa zao la karafuu umeongezeka kufikia tani 3,072.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 1,691 za mwaka 2019 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 81.7. Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa zao hili na kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora ya mikarafuu.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo takwimu zinaonesha ongezeko la uchinjwaji wa Ng'ombe kutoka tani 24,057 (2019) hadi kufikia 29,844 (2020), Mbuzi tani 2,317 (2019) hadi 7,868 (2020) na Kuku tani 120,288

(2019) hadi tani 709,930 (2020). Vilevile, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka trei 11,937,050 (2019) hadi trei 12,024,496 na maziwa kutoka lita 4,641,258 (2019) hadi lita 6,113,345 (2020). (**Kiambatanisho Nam. 1C na 1D)**

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa misitu, takwimu zinaonesha mwaka 2020 matumizi ya kuni yamepungua kutoka mita za ujazo 27,496 ikilinganishwa na 32,189 za mwaka 2019, sawa na asilimia 15. Matumizi ya boriti (majengo) pia yamepungua kutoka mita za ujazo 1,721 mwaka 2019 hadi 1,450 mwaka 2020 sawa na asilimia 16. Uzalishaji wa nguzo kubwa umeongezeka kutoka mita za ujazo 3,115 mwaka 2019 hadi kufikia mita za ujazo 3,255 mwaka 2020 sawa na asilimia 5. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kujengea nao pia umeongezeka kutoka mita za ujazo 2,790 mwaka 2019 hadi kufikia mita za ujazo 2,878 mwaka 2020 sawa na asilimia 3. Kwa ujumla matumizi ya nishati ya kuni yamepungua kutokana na juhudi inayochukuliwa na Serikali za kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala (gesi na majiko sanifu) na utoaji wa taaluma katika uhifadhi misitu ya jamii. (**Kiambatisho Nam. 1E**).

## UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021

20. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mipango Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Z-ASDP). Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wakulima,

wafugaji na jamii jambo ambalo limeongeza ari na hamasa na hatimae kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, mifugo, kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora, ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

## MUUNDO WA WIZARA NA UTEKELEZAJI (2020/2021)

21. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali ya Awamu ya Nane uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inasimamia Idara sita (6), Taasisi mbili (2) za utafiti, Wakala wa Matrekta na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

- i Idara ya Kilimo na Uhakika wa chakula
- ii Idara ya Umwagiliaji Maji
- iii Idara ya Maendeleo ya Misitu
- iv Idara ya Maendeleo ya Mifugo
- v Idara ya Uendeshaji na Utumishi
- vi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
- vii Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo
- viii Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI)
- ix Tasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI)
- x Ofisi Kuu ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo – Pemba.

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu Nne ambazo ni:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu

3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

23. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Wizara iliendelea na kusimamia utekelezaji wa Mradi minne ya Maendeleo ikiwemo Mradi wa Uendelezaji wa Zao la Mpunga ERPP, Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu katika mazao ya nafaka TANIPAC, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na Mradi wa Kudhibiti Nzi waharibifu wa Matunda.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

24. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 10.47 bilioni kutoka vianzio vyake kumi na mbili (12). Aidha, kufuatia mabadiliko ya miundo ya Wizara, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imehamishiwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na kitengo cha Maliasili Zisizorejesheka kimehamishiwa Wizara ya Maji Nishati na Madini. Kwa mnasaba huo, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imebakiwa na lengo la kukusanya TZS 747,500,000 kupitia vyanzo vyake vinane (8) vya Unguja na Pemba.

Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi April, 2021 Wizara imekusanya jumla ya TZS.1.54 bilioni sawa na asilimia 206. Ongezeko la mapato limetokana na uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato katika vianzio vya mapato vya Wizara pamoja na usimamizi wa tozo mpya za mifugo. **(Kiambatanisho Nam. 3A)**.

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Wizara imeombewa kutumia jumla ya TZS 129.86 bilioni kati ya fedha hizo TZS 23.32 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.47 bilioni Mishahara na TZS 5.22 bilioni matumizi mengineyo na TZS 6.63 bilioni RUZUKU kutoka SMZ kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao Baharini, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara imeombewa TZS 106.54 bilioni (TZS 83.54 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 23.00 bilioni kutoka SMZ.

Kufuatia mabadiliko ya miundo ya Mawizara, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili, na Mifugo imebakiwa na TZS 102.8 Biloni (TZS 21.97 Bilioni kwa matumizi ya kawaida na TZS 80.86 Bilioni kwa kazi za maendeleo). **(Kiambatanisho Nam. 3B)**.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi April, 2021 Wizara imepata jumla ya TZS. 35.93 bilioni sawa na asilimia 35 ya fedha zilizoidhinishwa kati ya hizo TZS. 9.76 bilioni zimetumika kwa matumizi ya kawaida (TZS 8.19 bilioni mishahara; TZS 1.57 matumizi mengineyo) Ruzuku ya TZS 4.41 bilioni (TZS 3.48 bilioni mishahara na TZS 936.46 milioni kwa matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia April, 2021 Wizara imepata TZS 21.74 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Kiambatisho Nam. 3B)

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2020/2021

27. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

a) Wizara iliendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji maji katika hekta 1,524 ambapo; Ujenzi wa mabwawa matatu (3) katika mabonde ya Kinyasini na Chaani kwa Unguja na Mlemele Pemba unaendelea. Vilevile, ujenzi wa misingi mikubwa na midogo ya kumwagilia maji yenye urefu wa mita 5,170 bonde la Kinyasini, mita 10,630 bonde la Kibokwa na mita 2,440 katika bonde la Chaani umefanyika, pamoja na uchimbaji wa Visima 18 (Cheju 15, Kilombero 2 na Kibokwa 1).

b) Tani 244 za mbolea ya kukuzia (Urea), tani 50 za mbegu ya mpunga (SARO na TXD 88) na lita 12,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa msimu wa masika 2021 na kusambazwa kwa wakulima wa mpunga. Vilevile, tani 19 za mbolea ya kukuzia (Urea), tani 71 za mbolea ya kupandia – DAP na TSP tani 97 na lita 3,603 za dawa ya kuulia magugu zilizobakia mwaka wa fedha 2019/2020 zimesambazwa kwa wakulima. Jumla ya TZS. 98,344,850 (Unguja TZS. 65,919,850 na Pemba TZS. 32,425,800) zimekusanywa kutoka kwa wakulima ikiwa ni mchango wa Ruzuku ya pembejeo za kilimo zilizotolewa.

c) Ununuzi wa vifaa vya maabara na lita 400 za dawa ya kuulia nzi wa matunda (methyl eugenol) vyenye thamani ya Euro 26,705.6 sawa na TZS 73,707,456 Milioni vimenunuliwa kupitia Mradi wa Udhibiti nzi wa matunda unaotekelezwa baina ya Wizara na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (International Atomic Energy Agency).

d) Tathmini ya maradhi ya mnyauko wa migomba yanayosababishwa na "Fusarium" ilifanyika Uzi na Tumbatu Unguja na Kisiwa Panza, Fundo na Kojani Pemba. Matokeo ya awali yamebaini kuwepo kwa maradhi hayo ya aina mbili kati ya tatu zilizopo nchi za jirani katika migomba jamii ya koroboi, pukusa na Bukoba. Aina ya tatu ambayo haipo Zanzibar ni hatari zaidi kuliko hizo mbili na hii inaathiri migomba ya aina zote. Wizara inaendelea na Karantini ya kuzuia uingizaji wa miche ya migomba na ndizi za aina zote hapa Zanzibar kutoka nchi jirani;

e) Jumla ya miche 987,743 (minazi 71,140, mikarafuu 340,920 na matunda na viungo 44,741, miche ya misitu 530,942) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali na kusambazwa kwa wakulima.

f) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ZARI) imeendelea kufanya Tafiti saba (7) za kilimo kwa mazao ya mpunga, mboga, muhogo, viazi vitamu na migomba. Kwa upande wa mpunga na mazao ya mizizi tafiti zilijikita kwenye kutafuta mbegu bora zinazostahamili maradhi ya Rice Yellow Mottle Virus na Rice Blast kwa mpunga na ya mchirizi ya kahawia (Cassava Brown Streak Disease) kwa muhogo. Majaribio ya matumizi ya mbolea ya vidonge (UDP) kwa mazao ya mboga za mchicha, nyanya chungu na tungule yaliendelea. Utafiti wa uzalishaji wa miche aina migomba na Mikaratusi (Eucalyptus) kwa njia ya chupa (tissue culture) na utafiti wa kutumia maji ya moto kudhibiti minyoo ya migomba ulifanyika. Mafanikio ya tafiti hizi ni kuongeza uzalishaji wa mbegu na miche bora itakayostahamili maradhi, wadudu na mabadiliko ya tabianchi na hatimae kuongeza uzalishaji.

g) Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa kuendeleza zao la nazi ambapo Sera na Sheria zimetayarishwa pamoja na

kuendelea na mkakati wa kudhibiti biashara ya madafu ya minazi ya asili (East African Tall). Juhudi hizi zimeanza kutoa matunda kwa kuongezeka kwa uzalishaji wa nazi na kushuka kwa bei ya zao hilo;

h) Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo imetoa huduma za uchimbuaji na uburugaji wa ardhi kwa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua katika ekari 10,043.5 (Unguja 7,542.50 na Pemba 2,501.00) kwa kutumia matrekta 42 (26 Unguja na 16 Pemba). Aidha, Wakala imepokea mchango wa mafuta kutoka kwa wakulima jumla ya TZS.91,968,750 (Unguja TZS.61,331,750 na Pemba TZS. 30,637,000)

i) Watalii 23,625 wa nje na ndani ya nchi walitembelea katika Hifadhi za Misitu za Jozani, Masingini na Ngezi Vumawimbi. Aidha, jumla ya TZS 742,987,036 zimepatikana kutokana na watalii hao;

j) Utafiti wa kujua idadi ya Paa nunga umefanyika katika Hifdahi ya Taifa Jozani Ghuba ya Chwaka na hifadhi ya jamii Mtende. Matokeao yanaonesha kuwepo paa Nunga 120 katika hifadhi ya Taifa na Paa nunga 95 katika hifadhi ya jamii Mtende. Aidha, paa wengine wanaoshabihiana nao walihesabiwa (Paa chesi na Paa Suni). Idadi ya Paa chesi ilikuwa 1,400 na Paa suni 756 katika hifadhi ya Taifa.

k) Jumla ya Ng'ombe 1,190 (Unguja 738 na Pemba 452) wamepandishwa kwa njia ya sindano, ambapo Ng'ombe 785 sawa na asilimia 66 wameshika mimba. Idadi hiyo inatarajiwa kuzalisha Ng'ombe wa maziwa wanaotoa wastani wa lita 10 za maziwa kwa siku;

l) Jumla ya Mbwa 8,028 na Paka 466 (Unguja mbwa 6,351 na paka 430 na Pemba mbwa 1,632 na paka 36)

wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha Mbwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Vilevile, Jumla ya Kuku 42,463 wamechanjwa dhidi ya maradhi ya Mahepe 35,634, Gumboro 3,605, Ndui 2,029 na Marek's 1,195 (Unguja 25,191 na Pemba 14,873). Jumla ya Ng'ombe 1,745 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu na kimeta (Anthrax), Ng'ombe 1,503 wamechanjwa chanjo ya maradhi ya miguu na midomo (Foot & Mouth Disease), Ng'ombe 142 na ugonjwa wa mapele ya ngozi (Lumpy Skin Disease). Hatua hii imetuwezesha kupunguza maradhi ya miripuko ya mifugo nchini.

m) Jumla ya sampuli 509 (Unguja 365 na Pemba 144) kutoka kwa Ng'ombe, Mbwa na Kuku zimechunguzwa maradhi, kati ya hizo sampuli 240 zimeonekana maradhi ya Ndigana kali 78 (East Coast Fever), kichaa cha mbwa 18 (Rabies), Minyoo100, ugonjwa wa kiwele 30 (Mastitis), ugonjwa wa mkojo mwekundu 2 (Babesiosis), ugonjwa wa kuharisha kwa kuku 12 (Coccidiosis). Aidha, Wizara imeweza kuwatibu wanyama hao kutokana na maradhi yaliyoonekana na kupunguza maambukizi.

n) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI) iliendelea na ufanyaji wa tafiti tatu (3) ikiwemo utafiti wa uzalishaji wa kuku wa kienyeji uliojumuisha kuku kishingo, kuchere, kibete kwa lengo la kuhifadhi mbegu za kienyezi zisipotee. Vilevile, Taasisi imefanya Utafiti wa mbuzi chotara watakao himili mazingira ya Zanzibar na utoaji wa maziwa kwa wastani wa lita mbili kwa siku. Aidha, Chotara hao wametokana na mbuzi wa asili (Small East African Goat) na aina ya Saannen na Toggernburg kutoka Arusha. Utafiti wa kujua aina na madhara ya kupe kwa ng'ombe wa maziwa na wa kienyeji katika wilaya sita za Zanzibar ikiwemo Wete, Micheweni, Mkoani, Kaskazini B, Magharibi B na Kati umefanyika. Aidha, utafiti

umeonesha kuna kupe wa aina 3 na utafiti unaendelea kwa lengo la kupata muongozo wa kupata dawa muafaka.

o) Wizara imeendelea na utoaji wa stahiki za wafanyakazi **591** kwa thamani ya **TZS. 85,580,576** ambapo wafanyakazi 224 wamelipwa fedha zao za likizo jumla ya TZS 22,400,700,000 (TZS.20,400,000 Unguja na TZS. 2,000,000 Pemba), wafanyakazi 323 wamelipwa malipo yao ya muda wa ziada jumla ya TZS 49,680,576 (TZS. 27,635,003 Unguja na TZS. 22,045,573 Pemba) na Ubani kwa wafanyakazi 44 kwa thamani ya TZS.13,500,000 (TZS. 11,100,000 Unguja na TZS.2,400,000 Pemba)

p) Wafanyakazi 18 wamelipiwa masomo na Wizara katika kada tofauti ikiwemo Shahada ya kwanza 15, Stashahada 2 na Stashahada ya Uzamivu 1. Vile vile, wanafunzi 32 wanaosomeshwa Shahada ya kwanza ya utibabu wa wanyama nchini China wameendelea kulipiwa masomo yao kupitia Bodi ya mikopo ya elimu ya juu na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Aidha, watumishi 18 wamejiunga na masomo katika kada tofauti ambao wanajilipia wenyewe katika vyuo tofauti vya Tanzania na Uganda. Wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa udhamini wa masomo ya Shahada ya Uzamivu na Uzamili kupitia mradi wa Kudhibiti Sumu Kuvu.

q) Jumla ya nakala 100 za Mpango Mkakati wa Ukusanyaji wa Takwimu za Sekta ya Kilimo na nakala 100 za Kitabu cha Mwenendo wa Takwimu zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau kwa lengo la kupata uelewa wa mwenendo wa takwimu za uzalishaji wa mazao na mikakati iliyowekwa katika kuimarisha ukusanyaji wa takwimu.

r) Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Mapokezi ya Watalii katika Msitu wa Hifadhi wa Ngezi Pemba lenye thamani

ya TZS. 250.31 milioni. Jambo ambalo litapelekea kuimarika kwa utalii, ongezeko la mapato na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

s) Kuanzishwa kwa mfumo maalum wa mawasiliano unaojuulikana kwa jina la Sema na Rais Mwinyi (SNRMwinyi) uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein A. Mwinyi, Mfumo huu umeiwezesha Wizara kuzifahamu changamoto za kiutendaji kwa haraka na kuweza kushughulikia na kutatua kero za wananchi. Jumla ya malalamiko 22 yamewasilishwa katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuanzia mwezi Febuari 2021 na yamepatiwa ufumbuzi wake.

t) Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uwekezaji na Kukuza Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) inaendelea kupokea wawekezaji waliojitokeza katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji maji, mazao ya mboga na matunda, viungo na katika sekta ya mifugo ikiwemo ujenzi wa machinjio ya kisasa, uzalishaji wa vifaranga vya kuku na uwekezaji katika misitu ya Jozani, Masingini na Kiwengwa.

u) Wizara imetia saini Mkataba wa makabidhiano ya maeneo ya sekta ya kilimo yaliyogatuliwa kwa ajili ya kuleta ufanisi na maendeleo ya sekta ya kilimo nchini. Maeneo yaliyorejeshwa yamejumuisha, Misitu ya jamii, Maafisa ugani, Vituo vya afya ya wanyama, Skimu za umwagiliaji maji na Vitalu vya miche kwa Unguja na Pemba.

## CHANGAMOTO

28. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

    a) Uvamizi wa ardhi za kilimo na misitu kutokana na kuongezeka kwa makaazi na miradi ya maendeleo;
    b) Uchelewaji wa wakulima kuchangia katika huduma za matrekta.
    c) Kuzorota kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;
    d) Kuzuka kwa maradhi ya Homa Kali ya Mapafu (Korona) inayosababishwa na virusi ya COVID-19, kumezorotesha ufanisi katika utekelezaji wa Mradi wa kudhibiti nzi wa matunda, ufinyu wa bajeti, ugumu wa upatikanaji wa vifaranga vya kuku na kuzuiliwa mafunzo na mikutano ya ndani na nje ya nchi.

## HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

a) Wizara inaendelea kuhamasisha jamii kupitia Halmashauri juu ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na uhifadhi. Vile vile, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inaendelea kuyapima na kuyapatia Hati Miliki maeneo ya Kilimo pamoja na kutenga ardhi ya akiba kwa ajili ya uwekezaji na uhifadhi kwa kizazi kijacho;
b) Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeandaa utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa fedha za mchango kwa ajili ya huduma za matreka, ambapo Wakala hufanya vikao vya pamoja kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya kuwahi msimu. Aidha, bado Wakala inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha hizo mwisho wa msimu

na kupelekea wakulima wengi kutaka huduma za matrekta kwa wakati mmoja kulingana na idadi ndogo ya matrekta yaliyokuwepo;

c) Wizara inaendelea kuchukua jitihada za kujadiliana na Mkandarasi pamoja na Mshauri elekezi ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi unakamilika kwa ubora na kwa wakati. Vilevile, Wizara inafanya ziara za mara kwa mara na vikao vya Kamati za uongozi na Kamati tendaji kila mwezi kwa kushirikiana na Benki ya Exim, mshauri elekezi, mkandarasi na Wizara za fedha za SMT na SMZ. Vile vile, Wizara imeshaiarifu Serikali na wadau juu ya changamoto za kiutendaji zinazoikabili mradi huo.

d) Wizara inaendelea kushiriki mafunzo na mikutano ya kikanda na kimataifa kupitia mitandao katika kukabiliana na athari za Korona. Vilevile, jumla ya wanafunzi 33 waliojiunga na masomo katika Chuo Kikuu cha YUCHIN cha China kwa Shahada ya kwanza ya Udaktari wa Vinyama kwa muhula wa mwaka 2018/2019 na 2019/2020 ambao hawajaenda China kutokana na Maradhi ya Korona wanaendelea na masomo ya lugha kupitia mtandao. Aidha, Wizara imeandaa darasa na kununua vifaa kwa ajili ya kufanikisha masomo hayo. Chuo Kikuu cha YUCHIN kimekubaliana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na WKUMM kuendesha masomo hayo ya lugha kwa kipindi cha miezi sita. Vilevile, Wizara imeshapeleka maombi katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kwa ajili ya kupata usimamizi wa mafunzo hayo katika Skuli ya Sayansi ya Kilimo.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA 2020/2021

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu nne ambazo ni:

    i. Programu ya Maendeleo ya Kilimo
    ii. Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka;
    iii. Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
    iv. Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

30. **Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu hii ni kusimamia matumizi sahihi ya pembejeo na utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima, ikiwemo utoaji wa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao. Aidha, programu ina jukumu la kusimamia na kuendeleza tafiti za kilimo na maliasili pamoja na upatikanaji wa huduma za matrekta na zana za kilimo

    Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo imegawika katika programu ndogo tano (5) ambazo ni:

    a. Programu ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji;
    b. Programu ndogo ya Utafti na Mafunzo ya Kilimo;
    c. Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo;
    d. Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo;
    e. Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

31. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na muundo mpya wa Wizara, Programu ndogo ya Uhakika wa Chakula imeunganishwa katika Programu Ndogo ya Maendeleo ya Kilimo.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Kilimo iliidhinishiwa jumla ya TZS 79.03 bilioni kati ya fedha hizo TZS 5.57 kwa kazi za kawaida (TZS 2.39 bilioni ni Mishahara na TZS 3.17 bilioni matumizi mengineyo),. Wizara pia imeidhinishi wa kupata Ruzuku ya TZS 5.21 bilioni (TZS 3.17 bilioni ni Ruzuku ya Mishahara na TZS 2.03 bilioni matumizi mengineyo) kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Programu pia imeidhinishiwa TZS 68.24 bilioni kwa miradi ya maendeleo (TZS 48.24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 20.00 bilioni kutoka SMZ). Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata TZS. 26.47 bilioni sawa na asilimia 33 (TZS. 6.15 bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS. 20.31 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo)

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji**

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 programu ndogo hii imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

**a.** Ujenzi wa misingi mikubwa na midogo ya kumwagilia maji yenye urefu wa jumla ya mita 5,170 (5,17km) katika bonde la Kinyasini, mita 10,630 katika bonde la Kibokwa na mita 2,440 katika bonde la Chaani umefanyika. Aidha, ujenzi wa culvert za kupitishai maji katika mabonde ya Chaani, Kibokwa na Kinyasini umefanyika

- Uchimbaji wa misingi mikubwa na midogo ya kutolea maji katika ploti (Drainage canals)

mabonde ya Chaani, Kibokwa, Kinyasini, Kilombero na Cheju umekamilika.

- Ujenzi wa Pokezi la maji (intake tunnel) na miundombinu ya kutolea maji ya ziada kwenye mabwawa (spillway) katika mabonde ya Chaani na Kinyasini umekamilika.
- Uchimbaji wa visima vinane (8) pamoja na kufanya majaribio ya utokaji wa maji katika mabonde ya Kilombero Cheju na Kibokwa. Aidha, Kazi za uwekaji sawa wa ploti (leveling) pamoja na utengenezaji wa matuta ya misingi ya maji na njia za mabondeni (Farm roads) katika mabonde ya Kilombero, Kinyasini na Cheju zimeendelea.
- Utengenezaji wa matuta (Canal Embankment) kwa ajili ya ujenzi wa mitaro ya umwagiliaji (Irrigation Cannal) katika bonde la Kibokwa, Chaani, Kinyasini, Cheju na Kilombero umefanyika.
- Uwekaji sawa (Leveling) wa ploti na utengenezaji wa matuta ya block katika mabonde ya Kibokwa, Chaani, Kilombero na Kinyasini umefanyika.

**b.** Kazi za awali za utambuizi wa wakulima wanaolima bonde la Cheju na Kilombero zinaendelea pamoja na kazi za uhakiki kwa kupata takwimu sahihi;

**c.** Kazi za uimarishaji wa jumuiya za wakulima zinaendelea kwa kushirikiana na Halmashauri husika katika mabonde ya Bumbwisudi, Cheju, Mtwango, Kibokwa, Kibondemzungu, Mchangani na Koani. Aidha, Idara ilisimamia uchaguzi mkuu wa jumuia ya wakulima katika bonde la Bumbwisudi.

- Kazi ya uchunguzaji na marekebisho ya tatizo la umeme katika visima vitatu (3) vya Bumbwisudi (Mkanyageni, Langoni na Kati) imefanyika.
-

- Kazi ya ubadilishaji wa mabomba ya chuma (G1) na uwekaji wa mabomba ya plastic aina ya HDPP katika kisima cha Cheju (TASSAF Ndijani) - imefanyika.
- Kazi ya ujenzi wa Barabara ya shambani (Farm road) yenye urefu wa kilomita 1.5 kwa kiwango cha kifusi bonde la Bumbwisudi-Kirundunda umekamilika.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii imeidhinishiwa jumla ya TZS 67.96 bilioni ambapo (TZS 563.91 milioni Mshahara, TZS 312.57 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 67.09 bilioni fedha za maendeleo (TZS 19.90 bilioni kutoka SMZ na TZS 47.19 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK). Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata jumla ya TZS 20.47 bilioni sawa na asilimia 30 ya fedha zilizoombwa. Kati ya fedha hizo TZS 422.86 milioni kwa kazi za kawaida ikiwemo TZS 393.52 milioni mishahara na TZS 29.34 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 20.05 bilioni kwa kazi za maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK ya Korea.

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar**

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

    a. Tafiti za kilimo ziliendelea kufanyika kwa mazao ya mpunga, mboga, mazao ya mizizi (muhogo, viazi vitamu na vikuu) na migomba. Kwa upande wa mpunga na mazao ya mizizi tafiti zilijikita kwenye kutafuta mbegu bora zinazostahamili maradhi (Rice Yellow Mottle Virus, Rice Blast kwa mpunga na

Cassavaa Brown Sreak Disease kwa muhogo). Kwa mboga mboga majaribio ya matumizi ya mbolea ya vidonge (UDP) kwa mboga za mchicha, nyanya chungu na tungule yaliendelea. Utafiti wa uzalishaji wa miche aina mbali mbali kwa njia ya chupa (tissue culture) na utafiti wa kutumia maji ya moto kudhibiti minyoo ya migomba ulifanyika.

b. Uungwaji wa maji kwa eneo la shamba mama la migomba (Pemba) inayotumia umwagiliaji maji kwa njia ya matone umekamilika kwa asilimia 90. Kisima kimoja kimechimbwa Kizimbani na kuanza kutoa huduma

c. Uwekaji wa uzio kwenye eneo la urefu wa mita 350 katika shamba la viungo (spice farm) umetekelezwa. Ujenzi wa vyoo na sehemu ya mapokezi ya wageni na watalii upo katika hatua za mwisho.

d. Wafanyakazi sita wanapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi mbali mbali ndani ya nchi na wafanyakazi wanne wanapata mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi (Kampala University);

e. Ukarabati wa ofisi kuu Kizimbani ikijumuisha na ujenzi wa eneo la kuegesha magari na uwekaji wa bustani mbele ya jengo la utawala umekamilika. Ukarabati wa nyumba za wafanyakazi na ununuzi wa gari na pikipiki haukufanyika.

f. Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (2014 – 2019) umefanyiwa mapitio kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Tume ya Mipango.

g. Mazungumzo ya mashirikiano na Taasisi iitwayo "World Vegetable Research" yenye Afisi kuu Arusha yamefanyika kwa lengo la kusaidiana nao kitaaluma na kiufundi.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliidhinishiwa Ruzuku jumla ya TZS 3.05 bilioni (TZS 2.39 bilioni Mshahara na 660.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS 2.26 bilioni sawa na asilimia 74 (TZS 2.11 bilioni Mshahara na 151.84 milioni kwa matumizi mengineyo).

### Programu Ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula

37. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

   **a.** Tani 244 za mbolea ya kukuzia (Urea), tani 50 za mbegu ya mpunga (SARO na TXD 88) na lita 12,000 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa msimu wa masika 2021 na kugaiwa kwa wakulima wa mpunga. Aidha, tani 19 za mbolea ya kukuzia (Urea), tani 71 za mbolea ya kupandia – DAP na TSP tani 97 na lita 3,603 za dawa ya kuulia magugu zilizobakia mwaka wa fedha 2019/2020 ziligaiwa kwa wakulima.
   **b.** Vikao vya mashauriano ya pamoja na Wakurugenzi Wasaidizi wa Manispaa na Halmashauri za Wilaya vilifanyika Wilaya husika kwa lengo la kupanga mikakati ya uendeshaji mafunzo kwa msimu wa 2020/2021. Masuala makubwa yaliyojitokeza ni upatikanaji wa pembejeo kwa mujibu wa mapendekezo ya kitaalamu;
   **c.** Jumla ya ekari 10,329.5 (1,558.5 Unguja na 8,771 Pemba) zimeshachimbuliwa kwa matrekta na mkono.
   **d.** Kazi ya upandaji na utunzaji mbegu katika vituo vya kilimo Mwera eka 0.5 ya mbegu mama ya viazi vitamu, Bambi eka 2 za muhogo na Msaani eka 1.5 zinaendelea.
   **e.** Jumla ya tani 62,423.45 za mazao ya kilimo kutoka na kwenda Tanzania Bara na nje ya nchi yamekaguliwa kwa

lengo la kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao.

f. Utoaji taaluma ya kilimo hai kwa wakulima viongozi 50 (30 Unguja na 20 Pemba) kwa zao la tangawizi umefanyika.

g. Jumla ya watendaji 6 (wanaume 2 na wanawake 4) walipatiwa mafunzo ya siku tatu (3) ya uchambuzi wa taarifa za usalama wa chakula na lishe kwa kutumia "Special Package for Social Science" (SPSS) hapo Mazizini ofisi ya Chakula na lishe; Aidha, ufukizaji wa ghala kwa ajili ya kuthibiti wadudu waharibifu umefanyika mara 3 kila baada ya siku 45 kwa mujibu wa taratibu za ufukizaji;

h. Watendaji 5 wa Idara ya chakula na lishe wameshiriki mikutano miwili ya ukamilishaji wa kazi ya kuandaa Food Based Dietary Guidelines (FBDG) message iliofanyika Morogoro;

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu iliidhinishiwa TZS 5.84 bilioni kati ya hizo TZS. 4.69 ni kwa matumizi ya kawaida (TZS 1.83 bilioni ni Mishahara na TZS 2.85 bilioni kwa kazi za kawaida), kwa fedha za Maendeleo ni TZS. 1.15 bilioni (TZS 100 milioni kutoka SMZ na TZS 1.05 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS. 2.36 sawa na asilimia 40 (TZS 1.48 bilioni ni Mishahara na TZS 612.33 milioni kwa matumizi mengineyo), kwa fedha za Maendeleo ni TZS. 262.11 milioni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

## Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

39. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

    **a.** Jumla ya matrekta 42 (Unguja 26 na Pemba 16) na zana zake yanaendelea na kazi ya kutoa huduma za uchimbuaji na uburugaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga cha Msimu wa 2020/2021

    **b.** Jumla ya eka 10,043.5 (Unguja 7,542.50 na Pemba 2,501.00) za wakulima zimelimwa na kuburugwa kwa ajili ya matayarisho ya kilimo cha Mpunga.

    **c.** Matengenezo makubwa ya matrekta na zana zake yameshindikana kufanyika kama ilivyopangwa. Hata hivyo, matengenezo madogo tu yamefanyika.

    **d.** Utaratibu wa kupata WATAALAMU kutoka Kampuni ya MAHINDRA & MAHINDRA kwa ajili ya kutoa mafunzo umekamilika.

40. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo hii imeidhinishiwa jumla ya TZS 2.16 bilioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 787.60 milioni ni mshahara na TZS 1.37 bilioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS 1.36 bilioni sawa na asilimia 63 (TZS 761.93 milioni ni Mishahara na TZS 605.24 milioni kwa matumizi mengineyo).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza raslimali

za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu na maliasili, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao sambamba na kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu.

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:

- Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu
- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka

Aidha Programu Ndogo ya Maliasili Zisizorejesheka imehamishiwa katika Wizara ya Maji, Nishati na Maadili.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu Kuu ya Maendeleo ya Misitu iliidhinishiwa TZS 5.84 bilioni ambapo TZS. 2.04 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.68 bilioni ni mishahara na TZS 359.35 milioni matumizi mengineyo) na TZS 3.80 bilioni kwa Miradi ya Maendeleo kutoka UNDP. Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata TZS.1.59 sawa na asilimia 27 (TZS 1.51 bilioni ni mishahara na TZS 83.17 milioni matumizi mengineyo).

## Programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu

44. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

**a.** Jumla ya Miche 505,160 (466,500 Unguja na 38,400 Pemba) ikiwemo 8,000 mikarafuu, 429,000 misitu, 33,770 matunda na viungo na Pemba 29,850 misitu, 5,850 matunda na 2,700 ya viungo;

b. Watalii 23,625 wa nje na wandani walitembelea katika Hifadhi za Misitu;

c. Jumla ya Doria 46 (29 Unguja na 17 Pemba) zimefanyika maeneo ya hifadhi za Misitu na Mashamba ya Serikali, ambapo matukio 22 ya uharibifu na usafirishaji wa rasilimali za Misitu bila kibali yaliripotiwa. Vilevile, msumeno wa moto mmoja (1) umekamatwa na kuhifadhiwa ghalani.

d. Utafiti wa kujua idadi ya Paa nunga umefanyika katika Hifdahi ya Taifa Jozani Ghuba ya Chwaka na hifadhi ya jamii Mtende. Matokeao yanaonesha kuwepo paa Nunga 120 katika hifadhi ya Taifa na Paa nunga 95 katika hifadhi ya jamii Mtende. Aidha, paa wengine wanaoshabiahina nao walihesabiwa (Paa chesi na Paa Suni). Idadi ilikuwa Paa chesi 1,400 na Paa suni 756 katika hifadhi ya Taifa. Aidha, kwa upande wa utafiti wa Popo wa Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 haukufanyika kutokana na uchache wa fedha

e. Jumla ya Tani 8.91 za Asali (Unguja 1.93 na Pemba 6.98) zimeripotiwa kuvunwa kwa msimu mdogo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu inajumuisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar na Programu Ndogo Mbili nazo ni:

- Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo
- Programu Ndogo ya Utibabu

Aidha Programu Ndogo ya Utibabu wa Mifugo imeunganishwa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Mifugo iliidhinishiwa TZS 3.68 bilioni ambapo TZS 2.68 bilioni kwa kazi za kawaida TZS. 1.54 (TZS 1.31 bilioni ni mishahara na TZS 233.66 milioni matumizi mengineyo) na Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo TZS.TZS 1.14 bilioni (TZS.519.60 milioni ni Mishahara na TZS.623.30milioni kwa matumizi mengineyo). Vilevile Programu imeidhinishiwa TZS.1.0 bilioni kwa Miradi ya Maendeleo kutoka SMZ. Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata TZS.1.93 sawa na asilimia 52 (TZS 1.69 bilioni ni mishahara na TZS 239.30 milioni matumizi mengineyo).

**Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo**

47. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

   **a.** Jumla ya eka 5 za malisho zimepandwa malisho aina ya Napier grass eka 3, Congo signal grass eka 1, Copra grass 0.5 eka na Guatamala grass 0.5 eka. Pia eka 4.5 za malisho aina ya napier grass na copra grass zimepaliliwa katika shamba la malisho Kizimbani – Unguja;

   **b.** Timu ya wataalumu wanne wa mifugo walienda Ngerengere Morogoro (Shamba la Uzalishaji Mitamba) kwa ajili ya kujifunza na tayari wameandaa andiko kwa ajili ya uzalishaji wa ng’ombe chotara wa maziwa Pangeni. Pia wawekezaji tayari wameonesha nia ya kuwekeza katika Shamba hilo;

   **c.** Kuwaunganisha wafugaji katika soko la maziwa na kiwanda cha Azam kupitia Jumuiya na vikundi vyao ambapo jumla ya lita 214,499 zimepatikana Unguja kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Febuari 2021;

   **d.** Jumla ya mbwa 11 na Paka 87 (Unguja mbwa 9 na paka 70 na Pemba mbwa 2 na paka 17) wamefugwa kizazi ili kupunguza idadi ya mbwa na paka wazururaji.

e. Jumla ya wanyama 19,107 waliogeshwa kwa dawa za kuulia kupe, chofuo na viroboto;
f. Jumla ya wanyama 62,074 waliugua na kutibiwa magonjwa mbalimbali kati ya hao Ng'ombe 8,855 Mbuzi/Kondoo 4,448 Mbwa 1,392 Paka 333, Kuku 45,925 Bata 709, Sungura 391 na Punda 21.

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Maendeleo ya Mifugo iliombewa jumla ya TZS 1.54 bilioni, kati ya fedha hizo (TZS 1.31 bilioni Mshahara, TZS 233.66 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata jumla ya TZS.1.14 bilioni sawa na asilimia 74 (TZS. 1.08 bilioni Mishahara na TZS.59.92 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar**

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Tafiti mbili (2) za Tathmini ya Kuku wa Kienyeji na Mbuzi wa Kienyeji na chotara zinaendelea.
b. Majaribio ya kulisha vyakula vilivyochanganywa mwani kwa kuku wa nyama yamefanyika. Majaribio kama haya yanatarajiwa kufanyika kwa wafugaji ili kupata matokeo katika mazingira tofauti.
c. Utafiti wa kupe katika Ngombe wa kienyeji na maziwa unaendelea

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, iliidhinishiwa TZS 2.14 bilioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 519.60 milioni ni mshahara na TZS 623.30 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 1.0 bilioni fedha za Maendeleo

kutoka SMZ). Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS 783.65 sawa na asilimia 37 (TZS 604.28 milioni ni mshahara na TZS 179.37 milioni kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAZI ZA WIZARA YA KILIMO.**

51. **Mheshimiwa Spika,** dhumuni la Programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti, pamoja na kuratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje. Aidha, programu hii pia inasimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu.

Programu imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:

- **a.** Programu ya Utawala na Uendeshaji;
- **b.** Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti;
- **c.** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Kazi za Kilimo Maliasili na Mifugo Pemba.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa jumla ya TZS 14.26 bilioni kati ya hizo TZS 6.45 bilioni (TZS 5.30 bilioni ni mshahara, TZS 1.15 matumizi mengineyo) na TZS 7.81 kwa ajili ya kazi za Miradi ya Maendeleo kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata jumla ya TZS.5.93 bilioni sawa na asilimia 42 (TZS. 3.70 bilioni Mishahara, TZS.788.98 milioni matumizi mengineyo na TZS. 1.43 bilioni kwa miradi ya maendeleo kutoka Benki ya Dunia.

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

- **a.** Wafanyakazi 591 wamepatiwa stahiki zao zenye thamani ya TZS.85,580,576;
- **b.** Wafanyakazi 18 (1 PGD, 15 Degree na 2 Diploma) wamelipiwa masomo na Wizara katika kada tofauti; Pia watumishi 18 wamejiunga na masomo katika kada tofauti ambao wanajilipia wenyewe, pamoja na wanafunzi 32 wanaosomeshwa Degree ya Veterinary Medicine nchini China;
- **c.** Kufuatilia ukodishwaji wa miembe katika shamba la Pangeni na Kibokwa kwa thamani ya TZS.12,200,000 pamoja na kufatilia utatuzi wa mgogoro wa shamba la wakfu na kesi ya migogoro wa ardhi Fuoni.
- **d.** Vikao 12 vya bodi ya Zabuni, vikao na ziara 3 za ukaguzi wa hesabu wa ndani na kikao kimoja cha kamati ya ukaguzi wa Wizara vimefanyika;
- **e.** Uboreshaji wa tovuti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kutoa taarifa za matukio katika vyombo vya habari zinazohusiana na sekta ya Kilimo pamoja na utengenezaji wa barua pepe za watumishi wa Wizara zipo kwenye hatua za awali.
- **f.** Ununuzi wa vifaa ikiwemo Komputa, Spika na Hard disk kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa SNRMwinyi kwa lengo la kuleta ufanisi katika kutatua malalamiko yanayowasilishwa katika sekta ya kilimo.
- **g.** Ununuzi wa Komputa na Projector kwa ajili ya kuendesha masomo kupitia mtandao (ONLINE) kwa wanafunzi 33 waliojiunga na masomo katika Chuo Kikuu cha YUCHIN cha China kwa fani ya Shahada ya kwanza ya Udaktari wa Vinyama kwa muhula wa mwaka 2018/2019 na 2019/2020 ambao hawajaenda China kutokana na Maradhi ya Korona.

54. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, imeidhinishiwa jumla ya TZS 2.36 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.82 bilioni ni mishahara na TZS 542.63 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS 1.65 sawa na asilimia 70 (TZS 1.16 bilioni ni Mishahara na TZS 482.3 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

**a.** Mapitio ya Sera ya Kilimo yamefanyika na imekamilika bado kuchapishwa;
**b.** Mapitio ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Kilimo yanaendelea, kwa kufuata muongozo uliotoka Tume ya Mipango;
**c.** Vikao vya maandalizi ya utayarishaji Mipango Mikakati ya Kilimo ya Wilaya vimefanyika;
**d.** Wizara imeshiriki mikutano na Taasisi tofauti za ndani, Tanzania Bara na kikanda, ikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, vikao vya SADC.
**e.** Ukusanyaji wa Takwimu na Sensa ya Kilimo Tanzania bara na Zanzibar na kuchapisha kitabu cha takwimu za sekta ya kilimo na Mpango Mkakati wa Takwimu za Sekta ya Kilimo.
**f.** Kukamilisha utafiti wa Matumizi ya Mkaapoa Zanzibar.
**g.** Kushiriki mafunzo ya ukusanyaji wa Takwimu kwa njia ya Mtandao

56. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Mipango iliidhinishiwa jumla ya TZS 8.38 bilioni kati ya hizo TZS

570.85 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 258.85 milioni mishahara, TZS 312.00 milioni kwa matumizi mengineyo) na TZS 7.81 bilioni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi April, 2021 programu imepata jumla ya TZS 1.69 bilioni sawa na asilimia 20 (TZS. 219.17 milioni mishahara, TZS.36.71milioni matumizi mengineyo na TZS. 1.43 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo Benki ya Dunia

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili na Mifugo Pemba**

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya sekta ya kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ilitekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kufanikisha ziara na vikao vinne kwa Kamati ya Biashara, Kilimo na Utalii, Kamati ya PAC na Kamati ya Bajeti katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;
- **b.** Kufanya vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana idara na taasisi mbali mbali mtambuka za sekta ya kilimo-Pemba;
- **c.** Kuratibu ziara za wageni na viongozi wa Wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuhudhuria katika sherehe na kumbukumbu za kitaifa Unguja na Pemba;

**d.** Mashirikiano na taasisi nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii yameimarishwa.

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Programu hii iliidhinishiwa TZS 3.52 bilioni (TZS 3.22 bilioni mishahara na TZS 295.37 milioni ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi April, 2021 Programu imepata jumla ya TZS 2.59 bilioni sawa na asilimia 74 (TZS 2.32 bilioni ni Mishahara na TZS 269.9 milioni kwa kazi za kawaida.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### Makadirio ya Mapato

60. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 4.00 bilioni** kupitia vianzio vyake 11 viliopo Unguja na Pemba. **(Kiambatanisho Nam. 3C)**

### Makadirio ya Matumizi 2021/2022

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugokwa mwaka wa fedha 2021/2022, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 53.70** bilioni kati ya fedha hizo jumla ya TZS **17.16** bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 12.62 bilioni Mishahara na TZS 4.56 bilioni matumizi mengineyo). Aidha, jumla ya TZS **6.63** bilioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

(TZS 3.88 bilioni Mishahara na TZS 2.75 bilioni matumizi mengineyo). **(Kiambatanisho Nam. 3D)**

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya TZS **29.86** bilioni (TZS 23.88 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 5.98 bilioni kutoka SMZ). **(Kiambatanisho Nam. 3D)**

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake nne kuu kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

64. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa Miradi mitatu (3) ya Maendeleo ikiwemo Mradi wa kudhibiti Sumu Kuvu (TANIPAC), Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na Mradi wa kudhibiti Nzi wa Matunda (Kiambatisho Nam. 6A-6G)

## MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara ya Kilimo, Uwagiliaji, Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

1) Kuhamasisha ***kilimo biashara*** katika mazao ya viungo, mboga na matunda, mpunga, mazao ya mizizi na miwa

kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ikiwemo mbinu bora za ***Kilimo Hai***, ili kuongeza uzalishaji wenye tija na uhifadhi wa mazingira.

2) Kutoa huduma za matrekta katika ekari 17,400 (Unguja 9,000 na Pemba 8,400) na kuhamasisha matumizi bora ya pembejeo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.
3) Ujenzi wa maghala mawili (2) ya hifadhi ya chakula yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2000 kila moja, pamoja na chinjio la kisasa Kisakasaka
4) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 453 na kufanya matengenezo ya skimu nne za umwagiliaji maji katika maeneo ya Bumbwisudi na Cheju kwa Unguja na Saninga na Machigini kwa Pemba.
5) Kuhifadhi Misitu ya asili na ya jamii pamoja na kuimarisha shughuli za Utalii katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa na kuendeleza uwindaji wa kitalii katika misitu ya jamii iliopo Mtende na Muyuni.
6) Kuotesha kibiashara miche ya Mikarafuu 500,000, Minazi 500,000, Misitu 800,000 na miche ya matunda na viungo 400,000;
7) Kutoa chanjo dhidi ya maradhi ya miripuko kwa ng'ombe 30,000; kuku 200,000 na mbwa 8,000 pamoja na kupandisha ng'ombe 2,000 kwa njia ya sindano
8) Kuendeleza tafiti za kisayansi 11 (9 Kilimo na Mifugo 2) zinazoendelea na tafiti saba mpya (3 Kilimo na 4 Mifugo) pamoja na tafiti za kutatua changamoto za kijamii mbili na kuimarisha miundombinu ya utafiti na kuwajengea uwezo watafiti wa sekta ya kilimo;
9) Kutoa maslahi kwa Wafanyakazi 1,060, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 20 na vijana 50 wanaoendelea na masomo ya Udaktari wa mifugo nchini China pamoja na vyuo vyengine;

10) Kupitia Sheria 2 (Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999, Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996), pamoja na Kanuni 3 ikiwemo Misumeno ya Moto 2015, Uhifadhi wa Msitu ya Kimaumbile 2018 na Kanuni ya Ada na Tozo ya mazao ya Misitu 2013.
11) Kusimamia utekelezaji wa program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;
12) Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Sekta ya Kilimo;

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO

66. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inazo programu ndogo mbili**:**

i. Kuendeleza miundombi ya Umwagiliaji maji
ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 37.30** bilioni ambapo kati ya hizo **TZS 5.15** bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 2.86 bilioni Mshahara, TZS 2.29 bilioni kwa matumizi mengineyo), TZS **5.24** bilioni ikiwa ni Ruzuku (TZS 3.17 bilioni Mshahara, TZS 2.07 bilioni kwa matumizi mengineyo) kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, programu inaombewa**TZS 26.90** bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (TZS 23.88 bilioni kutoka EXIM BANK ya Korea na TZS 3.020 bilioni kutoka SMZ).

**Programu Ndogo ya Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji**

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Uimarishaji na Usimamizi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji kwa Mwaka 2021/2022**

**a.** Kujenga na kusimamia miundombinu ya Umwagiliaji yenye ukubwa wa eneo la hekta 453 katika mabonde ya Cheju, Kilombero na Mlemele kupitia mradi wa (EXIM Bank) ya Korea.

**b.** Kushajiisha wakulima kuchangia uendeshaji na kufanya matengenezo ya skimu za umwagiliaji maji katika mabonde 4 ya Bumbwisudi na Cheju kwa Unguja Machigini na Saninga Pemba;

**c.** Kuunga umeme wa njia kuu (Three Phase) katika mabonde matatu; Cheju, Kilombero na Kibokwa.

**d.** Kulipa fidia kwa wakulima 600 walioathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Kilombero na Mlemele.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 26.77** bilioni ambapo **TZS 979.62** milioni kwa kazi za kawaida (TZS 616.70 milioni Mshahara, TZS362.81 milioni kwa matumizi mengineyo). Vilevile, programu inaombewa**TZS 25.79** bilioni fedha za maendeleo (TZS 22.89 kutoka EXIM BANK ya Korea na TZS 2.90 bilioni kutoka SMZ).

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.**

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula Mwaka 2021/2022**

- **a.** Kununua na kusambaza tani 60 za mbegu ya mpunga, tani 300 za mbolea (TSP 100, UREA 150 na DAP 50) na lita 12,000 za dawa ya kuulia magugu;
- **b.** Kuendeleza zao la karafuu na nazi kwa kuotesha miche 500,000 ya mikarafuu (200,000 Unguja na 300,000 Pemba) miche 200,000 ya matunda na viungo, miche 500,000 ya minazi (300,000 Unguja na 200,000 Pemba).
- **c.** Kuimarisha kazi za karantini na ukaguzi wa mazao ya kilimo yanayoingia na kusafirishwa nje ya nchi.
- **d.** Kuwajengea uwezo wakaguzi wa mazao 40 juu mbinu bora za ukaguzi, mabwana/mabibishamba 200 juu ya mbinu mchanganyiko za udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu wa mazao na matumizi bora ya viuatilifu;
- **e.** Kujenga maghala mawili ya Hifadhi ya Chakula Unguja na Pemba na kufuatilia hali ya usalama wa chakula nchini;
- **f.** Kutoa elimu kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda, viungo na miwa.
- **g.** Kuhamasisha wawekezaji katika uzalishaji wa mazao ya kimkakati ikiwemo Mpunga, Mboga na matunda, mazao ya viungo na Miwa
- **h.** Kuhamasisha na kutoa taaluma juu ya Kilimo hai katika mazao ya Viungo, mboga na matunda.

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 5.28** bilioni ambapo **TZS 4.16** milioni kwa kazi za kawaida (TZS 2.24 bilioni Mshahara, TZS1.92 milioni kwa matumizi mengineyo).Vilevile, programu inaombewa **TZS 1.11** bilioni fedha za maendeleo (TZS 993.08 milioni kutoka Benki ya Dunia na TZS 120.00 milioni kutoka SMZ).

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

70. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inatekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2021/2022**

**a.** Kusimamia na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya matrekta na zana za kisasa za kilimo zitakazopelekea kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo;
**b.** Kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima, sekta binafsi na Taasisi nyengine;
**c.** Kuendeleza utoaji wa huduma za matengenezo ya matrekta na zana za kilimo za Serikali na sekta binafsi pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi na vipuri kwa ajili ya huduma;
**d.** Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kuchimba na kuburuga ekari 17,400 Unguja 9,000 na Pemba 8,400.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inaombewa jumla ya **TZS. 2.35 bilioni** kwa ajili ya ruzuku (TZS 842.30 milioni Mshahara, TZS 1.51 bilioni kwa matumizi mengineyo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI**

72. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Kilimo – ZARI inatekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula,

**Shabaha zitakazotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar –ZARI kwa mwaka 2021/2022**

73. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi ya Utafiti inalenga kutekeleza yafuatayo:

   **a.** Kufanya tafiti 12 za kilimo na maliasili (9 zinazoendelea na 3 mpya);

   **b.** Kuimarisha miundombinu ya utafiti kwa ununuzi wa vifaa vya maabara na madawa;

   **c.** Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 30 na mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 2 (1 Uzamili, 1 Uzamivu).

   **d.** Kuzalisha miche bora na salama ya migomba, Mihogo na Viazi vitamu kwa njia ya chupa (Tissue Culture) za kuisambaza kwa wakulima.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo – ZARI, inaombewa jumla ya **TZS 2.89** bilioni kwa ajili ya ruzuku (TZS 2.33 milioni Mshahara na TZS 560.80 milioni kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

75. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inayo programu ndogo moja ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Misitu

**Shabaha zitakazotekelezwa na programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu**

76. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

   **a.** Kuotesha miche 1,000,000 (misitu 800,000, matunda na viungo 200,000) pamoja na kujenga miundombinu ya vitalu 3;

b. Kupanda miti hekta 130 Unguja 90 na Pemba 40 (hekta 100 Mashamba ya Serikali 30 Mikoko) na kuhamasisha jamii kupanda miti katika mashamba, maeneo ya wazi na barabarani;
c. Kujenga mabanda matatu (3) ya mfano ya kufugia nyuki katika Wilaya ya Micheweni, Kusini na Kati pamoja na kutoa mafunzo ya ubora wa uzalishaji wa asali isiyokuwa na kemikali (Organic honey) kwa wakulima 300;
d. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika misitu ya hifadhi ya Jozani, Masingini, Kiwengwa na Ngezi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi kufikia 100,000;
e. Kufanya tathmini ya Misitu ya Jamii 53 na maendeleo ya miradi mbadala inayotumiwa na jamii katika maeneo ya hifadhi.
f. Kutoa mafunzo ya askari Usu 32 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika hifadhi ya Jozani Ghuba ya Chwaka, Kiwengwa, Masingini na Ngezi.
g. Kufanya doria 500 ili kudhibiti matukio ya uharibifu wa rasilimali za misitu na kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi na mashamba ya Serikali.
h. Kukamilisha utafiti wa kujua idadi ya wanyama adimu na mazingira yao wakiwemo Popo na Paa Chesi kwa Pemba.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Misitu inaombewa jumla ya TZS 2.76 bilioni ambapo (TZS 2.24 bilioni Mshahara na TZS 521.195 milioni kwa matumizi mengineyo).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

78. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inayo programu ndogo moja ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI)

**Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo Shabaha zitakazotekelezwa na Programu hii 2021/2022**

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kupandisha Ng'ombe 2,000 (Unguja 1,200, na Pemba 800) kwa njia ya sindano;
- **b.** Kuchanja Ng'ombe 30,000, kuku 200,000 na mbwa 8,000 dhidi ya magonjwa ya chambavu (BQ), kimeta, ugonjwa wa mapele ya ngozi na ugonjwa wa miguu, midomo, mahepe, gumboro, ndui na kichaa cha mbwa ;
- **c.** Kufunga uzazi mbwa 50 na paka 150 ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji.
- **d.** Ujenzi wa chinjio la kisasa Kisakasaka;
- **e.** Kutoa elimu ya ufugaji bora na uzalishaji wa Kuku, Ng'ombe na Mbuzi wa maziwa pamoja na Sungura

80. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo inaombewa jumla ya TZS 5.29 bilioni ambapo kati ya hizo TZS 2.32 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.63 bilioni mshahara na TZS 695.34 matumizi mengineyo). Aidha, programu inaombewa kutumia TZS 1.70 bilioni kwa kazi za Maendeleo kutoka SMZ kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Chinjio la Kisasa Kisakasaka.

### Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI

81. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI inatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Mifugo

### Shabaha Zitakazotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI 2021/2022

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    a. Kufanya tafiti 6, nne mpya na mbili zinazoendelea.
    b. Kupanda ekari 10 (Unguja 3 na Pemba 7) za malisho kwa ajili ya mbegu hifadhi na kuwapatia wafugaji.
    c. Kukamilisha ujenzi wa jengo la kiwanda cha chakula cha kuku, maabara, pamoja na ujenzi wa mabanda matatu ya utafiti wa Ng'ombe, Mbuzi na Sungura pamoja na ofisi Pemba.

83. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - ZALIRI inaombewa Ruzuku ya TZS 1.39 bilioni (TZS 706.30 milioni Mshahara, TZS 685.40 milioni kwa matumizi mengineyo). Vilevile, Taasisi inaombewa TZS 1.26 kutoka SMZ kwa kazi za Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa majengo ya Taasisi Unguja na Pemba).

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

84. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inazo programu ndogo tatu**:**

    i. Utawala na Uendeshaji
    ii. Mipango, Sera na Tafiti
    iii. Uratibu wa kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 6.94** bilioni kwa kazi za kawaida ambapo kati ya hizo TZS 5.89 bilioni mishahara na TZS 1.05 matumizi mengineyo.

**Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji 2021/2022**

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, huduma hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 1,060 na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;
- **b.** Kuendelea kuwalipia gharama za mafunzo wafanyakazi 20 wanaoendelea na vijana 50 wanaondelea na masomo ya Udaktari wa mifugo nchini China;
- **c.** Kudhibiti na kusimamia mali za Serikali;
- **d.** Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

87. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo inaombewa jumla ya **TZS 2.40** bilioni ambapo (TZS 1.91 bilioni Mshahara, TZS 488.02 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2021/2022**

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kupitia Sheria 2 (Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999, Sheria ya Usimamizi na

Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996), pamoja na Kanuni 3 ikiwemo Misumeno ya Moto 2015, Uhifadhi wa Msitu ya Kimaumbile 2018 na Kanuni ya Ada na Tozo ya mazao ya Misitu 2013.

**b.** Kutayarisha Mipango Mikakati ya Kilimo ya Wilaya na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;
**c.** Kufanya tafiti 2 za kiuchumi na Kijamii kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti ya Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo;
**d.** Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Takwimu;
**e.** Kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani, kikanda na kimataifa.

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya **TZS 612.731** milioni ambapo (TZS 328.66 milioni Mshahara, TZS 283.59 milioni kwa matumizi mengineyo).

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba**

**Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2021/2022**

**90. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

**a.** Kuratibu vikao na ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;
**b.** Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;
**c.** Kuratibu ziara za wageni na viongozi wa Wizara pamoja na kuhudhuria katika vikao, sherehe na kumbukumbu za kitaifa;

**d.** Kutatua changamoto za wadau pamoja na kuimarisha mashirikiano na taasisi nyenginezo (Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii).

91. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa OfisiKuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, inaombewa kutumia jumla ya **TZS 3.93** bilioni (TZS 3.64 bilioni mishahara na TZS 284.84 milioni ni matumizi mengineyo).

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

92. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 4.00** bilioni kupitia vianzio vyake tisa (9) viliopo Unguja na Pemba.

93. **Mheshimiwa Spika,**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 53.70** bilioni, kati ya fedha hizo **TZS 17.18** bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 12.62 bilioni Mishahara na TZS 4.56 bilioni matumizi mengineyo) na **TZS 6.63** billioni ni Ruzuku (TZS 3.88 bilioni Mishahara na TZS 2.75 bilioni matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa TZS **29.86** bilioni (TZS 23.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 5.98 bilioni kutoka SMZ).

## SHUKURANI

94. **Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, na mifugo zikiwemo Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji; Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Fedha na Mipango. Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Wizara ya Kilimo (SMT), Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT), CARI, Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT) na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT).

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatanguliza shukrani za dhati kwa Mashirika binafsi ya ndani, kikanda na Kimataifa ikiwemo ZSTC, TAHA, UWAMWIMA, COSTECH, TAFIRI, TALIRI, TPRI, Milele Foundation, Kilimo Trust, Zanchick, "ZAASO" na "ZSPCA". Vile vile nachukua fursa hii kwa kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza Kilimo, Mifugo na Uvuvi, zikiwemo Japan, China, India, Israel, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo nchini. Vilevile nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, ICRAF, IFAD, UNDP, FAO, JICA, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, CFC, WCS, GARC, "WHO", Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) na Umoja wa nchi za Ulaya - "EU"

96. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima, wafugaji na wanakamati za hifadhi za maliasili kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo ya chakula na biashara. Pia Napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini WKUMM, Wakurugenzi wa Maidara na Taasisi za Wizara na watumishi wote pasi na kuzisahau Halmashauri zote na wadau wote wa Sekta ya Kilimo, kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa Shabaha za Wizara hii mwaka 2020/2021.


97. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Ulinzi na Usalama, Baraza la Biashara la Taifa, Majukwaa ya Vijana, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu, Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

98. **Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe** nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.


**MHE. DKT. SOUD NAHODA HASSAN**
**WAZIRI, WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI,**
**MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**

## VIAMBATISHO


**Kiambatisho Nam. 1A**




**Kiambatisho Nam. 1B**




**Kiambatisho Nam. 1C**





| | Kuku/Bata | Ng'ombe | Mbuzi |
|---|---|---|---|
| 2020 | 711,590 | 29,844 | 7,868 |
| 2019 | 120,288 | 24,057 | 1,958 |

**Kiambatisho Nam. 1D**



**Kiambatisho Nam. 1E**



**Kiambatisho Nam. 2A**

**MRADI 1: KUIMARISHA UZALISHAJI WA MPUNGA (ERPP)**

| |
|---|
| Gharama za mradi kwa mwaka 2020/2021: Mradi uliombewa **TZS. 2,210,522,000** kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia Januari, 2021 fedha zilizopatikana kutoka Benki ya Dunia ni **TZS 1,437,589,874** |
| **Malengo ya Mwaka 2020/2021** |
| 1. Kuzalisha tani 10 za mbegu daraja la msingi kwa mashirikiano na Kitengo cha Mbegu.<br>2. Kutoa mafunzo kwa wakulima 100 ya uzalishaji mbegu kwa mkataba (24 Ole na 76 Kibondemzungu)<br>3. Kuandaa ziara za mafunzo Tanzania Bara kwa wakulima 60 na wakulima 46 baina ya Unguja na Pemba<br>4. Kuandaa mafunzo kwa wakulima 120 juu ya mbinu mchanganyiko za kudhibiti wadudu na maradhi ya mimea (IPM)<br>5. Kuandaa mafunzo ya Kilimo Shadidi kwa wakulima viongozi 40 Unguja na Pemba.<br>6. Kufuatilia miundombinu ya umwagiliaji baada ya kukamilika kazi za ujenzi kwa kipindi cha uangalizi miezi sita (6)<br>7. Kuandaa mafunzo kwa watumiaji maji katika skimu 20 za umwagiliaji |
| **Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2020/2021** |
| 1. Jumla ya tani 6.5 za mbegu daraja la msingi zimezalishwa.<br>2. Jumla ya wakulima 100 (24 Ole na 76 Kibondemzungu) wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji bora wa mbegu za mpunga.<br>3. Wakulima 35 (wanaume 17 na wanawake 18) walishiriki ziara ya mafunzo Morogoro.<br>4. Wakulima 31 (wanaume 11 na wanawake 20) walishiriki ziara baina ya Unguja na Pemba.<br>5. Wakulima 120 (wanaume 60 na wanawake 60) wamepatiwa mafunzo ya IPM kupitia mashamba ya maonesho 20 katika Skimu za Bandamaji, Kibondemzungu, Mchangani na Kianga kwa Unguja na Kwalempona, Machigini, Ole na Dobi kwa Pemba.<br>6. Wakulima viongozi 40 (wanaume 20 na wanawake 20) wa Skimu za Bandamaji, Kibondemzungu, Mchangani na Koani kwa Unguja na Kwalempona, Machigini, Ole na Dobi kwa Pemba wamepatiwa mafunzo ya Kilimo Shadidi cha Mpunga.<br>7. Ufuatiliaji umefanyika katika Skimu zote 7.<br>8. Mafunzu ya usimamizi na utunzaji wa Skimu yametolewa kwa wakulima 45 na Maafisa Ugani 18 kutoka Skimu 9 (Mtwango, Kibondemzungu, Koani, Bandamaji, Mchangani, Kwalempona, Ole, Dobi na Machigini). |
| **MRADI HUU UMEMALIZA MUDA WA UTEKELEZAJI** |

**Kiambatisho Nam. 2B**

**MRADI: MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI**

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka wa fedha **2020/2021** Mradi huu ulipangiwa **TZS 20.48 bilioni** kutoka SMZ kama mchango wa Serikali na **TZS 47.19** bilioni kutoka EXIM BANK ya Korea. Hadi kufikia Aprili 2021 mradi umepata **TZS 20.05** bilioni kutoka EXIM BANK ya Korea na haikupata fedha yoyote kutoka SMZ. |
| **Malengo kwa mwaka 2020/2021** |
| Usimamizi na Ufatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji utakaoendeleza hekta 600 katika mabonde ya Chaani, Kilombero na Cheju. Aidha, kazi za ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji katika mabonde ya Makwararani na Mlemele zitafanyika<br><br>Ulipaji wa fidia ya mazao kwa wakulima watakaoathirika wakati wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Chaani, Kinyasini, Cheju, Makwararani na Mlemele.<br><br>Utambuzi na Uhakiki wa Idadi ya wakulima katika mabonde yatakayoendelezwa miundombinu ya umwagiliaji yakiwemo Kilombero, Cheju, Makwararani na Mlemele. |
| **Utekelezaji wa Malengo 2020/2021** |
| Kazi za ujenzi na usimamizi wa mradi wa umwagiliaji maji zinaendelea katika mabonde sita kwa Unguja na Pemba, zikijumuisha ukamilikaji wa mabwawa mawili kwa upande wa Unguja (bwawa la Kinyasini na la Chaani) na kuanza kuhifadhi maji ya umwagiliaji maeneo hayo. Kwa upande wa bwawa la Mlemele liliopo Pemba, kazi ya ujenzi wa mlango wa kuchukulia maji kutoka kwenye bwawa (Intake tunnel) imekamilika pamoja na njia ya kuchukua maji ya ziada (Spillway) kutoka kwenye bwawa kwa ajili ya kuzuia mafuriko na kuendelea kazi ya uwekaji na ushindiliaji wa udongo wa ujenzi wa tuta la bwawa.<br><br>Aidha, kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ya maji zinaendelea na utekelezaji wake ikiwemo ujenzi wa misingi ya umwagiliaji maji, barabara za mashambani, misingi ya kutolea maji ya ziada, uwekaji sawa wa konde, ukataji na ugawaji wa konde, ujenzi wa matuta madogo ya kugawa konde ambapo kumeendelezwa kwa Chaani hekta **71**, Kilombero hekta **215** na Cheju hekta **314** na kufikiwa asilimia za kazi kama ifuatavyo; Chaani **(94.26%)**, Kilombero **(69.34%)** na Cheju **(24.29%)** na kwa ujumla kazi zote za mradi zimefikiwa asilimia 53.5 za utekelezaji wake.<br><br>Tathmini ya malipo ya fidia ya mazao ya wakulima imekamilika na jumla ya wakulima wasiopungua 600 katika mabonde ya Chaani, Kinyasini, Cheju, Makwararani na Mlemele ndio watakaolipwa fidia za miti na mazao itakayoathirika na utekelezaji wa mradi huu.<br>Kazi za upimaji wa mabonde yatakayoendelezwa miundombinu ya umwagiliaji maji ikijumuisha utambuzi na uhakiki wa idadi ya wakulima zimekamilika, katika bonde la Chaani kuna wakulima **645**, bonde la Cheju kuna wakulima **3,720** kwa upande wa mabonde ya Pemba ya Makwararani na Mlemele uhakiki unaendelea kwa hatua za mwishoni. |

**Kiambatisho Nam. 2C**

**MRADI: MRADI WA KUDHIBITI SUMUKUVU TANZANIA (TANIPAC)**

| |
|---|
| Gharama za mradi kwa mwaka 2020/2021: Mradi uliombewa **TZS 931,698,000** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia. Hadi kufikia April, 2021 fedha zilizopatikana ni **TZS 188,410,752,** |
| **Malengo ya Mwaka 2020/2021** |
| 1. Kudhamini wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu<br>2. Kufanya upembuzi wa uwelewa na mahitaji ya elimu ya sumukuvu kwa wakulima (training need assessment)<br>3. Kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari<br>4. Ununuzi wa mashine 2 za maabara kwa ajili ya kupima sumukuvu<br>5. Kushiriki katika maonesho.ya siku ya wakulima nanenane<br>6. Kutengeneza vifaa vya kutoa elimu(T-shirt, poster, leaflets nk)<br>7. Kufanya uchunguzi wa hali ya sumukuvu hapa Zanzibar<br>8. Ujenzi wa ghala za kuhifadhi nafaka |
| **Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2020/2021** |
| 1. wanafunzi wawili (2) wa shahada ya uzamili na wawili (2) shahada ya uzamivu tayari wameanza masomo katika vyuo vya Tanzania<br>2. Jumla ya watu 120 walihojiwa Unguja and Pemba. Ambapo wote kwa ujumla walikubali kwamba hili tatizo halielweki katika jamii na mafunzo ni muhimu yatolewe kwa wadau wote<br>3. Mafunzo yalifanyika Unguja na kuwashirikisha waandishi wa habari wa Unguja 10 na Pemba 5 pamoja na PSO wa mradi<br>4. Mkataba wa manunuzi umeshasainiwa na mashine zinatarajiwa kununuliwa na kukabidhiwa Taasisi husika<br>5. Mradi umeweza kutoa elimu ya kudhibiti sumukuvu katika maonesho<br>6. Fulana 200,kofia 2,000 vipeperushi 2,000 na flyers 2000 pamoja na mabango 2 zilichapishwa na kugawiwa<br>7. Michoro ipo tayari, wakandarasi wameshapatikana mchakato upo hatua ya kupata ruhusa ya mfadhili ADB kazi iweze kuanza |

**Kiambatisho Nam. 2D**

**MRADI: MRADI WA KUDHIBITI NZI WA MATUNDA**

| |
|---|
| **Gharama za mradi kwa mwaka 2020/2021:** Mradi uliombewa TZS**.120,000,000** kutoka Shirika la Mionzi Duniani (IAEA) na **TZS. 100,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizopatikana kutoka IAEA ni **TZS. 73,707,456.** |
| **Malengo ya Mwaka 2020/2021** |
| 1. Kufanya uzinduzi wa mradi (SMZ).<br>2. Kufanya mikutano miwili (2) ya mapitio ya maendeleo ya mradi (SMZ).<br>3. Kufanya mkutano wa mwaka - mapitio ya maendeleo ya mradi (SMZ).<br>4. Uandishi wa ripoti (SMZ).<br>5. Kupokea wataalamu watatu (3) kutoka nje (IAEA).<br>6. Kupeleka masomoni wataalamu watano (5) nje ya nchi (IAEA).<br>7. Ununuzi wa dawa ya kunasia nzi wa matunda (IAEA).<br>8. Ununuzi wa dawa ya kuulia nzi na vifaa vya kujikinga na kusambazia mitego (SMZ).<br>9. Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa nzi wa matunda (SMZ).<br>10. Kufuatilia na kuhudumikia mitego kwa ajili ya ufuatiliaji nzi wa matunda (SMZ).<br>11. Kuchunguza kiwango cha nzi wa matunda na bionomiki (bionomics) (SMZ).<br>12. Kufanya tathmini ya kiwango cha athari za nzi wa matunda kwa matunda yaliopo nchini (SMZ). |
| **Utekelezaji wa Malengo** |
| 1. Lita 400 za dawa ya kunasia nzi wa matunda imenunuliwa.<br>2. Vifaa vya maabara ya wadudu (specimen bottles na dissecting kits) zimenunuliwa.<br>3. Changamoto za COVID-19 zimesababisha kutokutekelezwa kwa mafunzo ya wataalamu pamoja na safari za wataalamu ambazo zina umuhimu mkubwa katika kuanzisha na kuendeleza kazi za msingi za mradi huu. |
| **Kwa mwaka 2021/2022:** Mradi unaombewa TZS**. 303,940,000** kutoka IAEA na **TZS 120,000,000** kutoka SMZ. |
| **Malengo kwa mwaka 2021/2022** |
| • Kufanya mikutano miwili (2) ya mapitio ya maendeleo ya mradi (SMZ)..<br>• Kufanya mkutano wa mwaka - mapitio ya maendeleo ya mradi (SMZ).<br>• Uandishi wa ripoti (SMZ).<br>• Kupokea wataalamu sita (6) kutoka nje (IAEA).<br>• Kupeleka masomoni wataalamu wawili (2) nje ya nchi (IAEA).<br>• Ununuzi wa vifaa vya GPS (IAEA).<br>• Ununuzi wa vifaa vya kukusanyia sampuli za wadudu na matunda (IAEA).<br>• Kununua vifa kwa ajili ya kampeni ya nzi wa matunda (SMZ/IAEA).<br>• Kufanya ziara za kimafunzo kwa viongozi (IAEA).<br>• Kufanya upembuzi yakinifu juu ya matumizi ya mbinu mchanganyiko katika maeneo maalumu (SMZ).<br>• Kukusanya matunda kwa utaratibu maalum (systematic fruit sampling) (SMZ). |

**Kiambatanisho Nam. 3A:**
**Jadweli la Upatikanaji wa Mapato Julai 2020 hadi April, 2021**

| Kasma Namba | Chanzo cha Mapato | Makadirio 2020/2021 | Makusanyo July hadi April | % |
|---|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | **394,000,000** | **92,488,400** | **47** |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 50,000,000 | 27,004,900 | 54 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 5,000,000 | 230,000 | 5 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 300,000,000 | 4,880,000 | 2 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 23,000,000 | 50,252,000 | 218 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 15,000,000 | 8,397,400 | 56 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 1,000,000 | 1,724,100 | 172 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | - | - | - |
| **JUMLA PEMBA** | | **394,000,000** | **92,488,400** | **23** |
| | | | | |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | **107,000,000** | **245,774,800** | **205** |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 100,000,000 | 244,084,800 | 205 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 7,000,000 | 1,690,000 | - |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | | | |
| | | | | |
| **IDARA YA KILIMO** | | **75,000,000** | **159,471,550** | **213** |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 75,000,000 | 159,471,550 | 178 |
| | | | | |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | **95,000,000** | **12,569,500** | **13** |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 15,000,000 | 9,288,500 | 59 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 60,000,000 | - | - |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 20,000,000 | 3,281,000 | 16 |
| | | | | |
| **IDARA YA MIFUGO** | | **76,500,000** | **1,032,355,808** | **1,349** |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 75,000,000 | 1,031,750,808 | 1,024 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 1,500,000 | 605,000 | 38 |
| | | | | |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | **-** | **-** | **-** |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | - | - | - |
| | | | | |
| **JUMLA UNGUJA** | | **353,500,000** | **1,450,171,658** | **410** |
| | | | | |
| **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | | **747,500,000** | **1,542,660,058** | **206** |

**NB: 1**
**KIFUNGU 1422048 - Ada Ukaguzi Wa Mazao Kinajumuisha Fedha Za Pembejeo:**

| | |
|---|---|
| PEMBA | 32,425,000 |
| UNGUJA | 65,919,850 |
| **JUMLA** | **98,344,850** |

**NB: 2**

| | VIANZIO VIPYA | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | 4,361,500 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | 738,625,536 |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA - PEMBA | 30,537,000 |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA - UNGUJA | 61,331,750 |
| **JUMLA** | | **834,855,786** |

**Kiambatanisho Nam. 3B:**

**JADWELI LA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULY 2020 HADI APRIL 2021**
**MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULY 2020 - APRIL 2021**

| Program kuu/ program ndogo | Makadirio 2020/2021 | Fedha iliyopatikana kwa kipindi cha july - april 2021 | | | | | | | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mshahara | Matumizi mengineyo | Ruzuku m/mengineyo | Ruzuku mshahara | Smz | Maendeleo muhisani | Jumla | |
| | | | | | | | | | |
| **PL0101 Maendeleo ya Kilimo** | **79,030,792,000** | **1,882,738,020** | **641,683,171** | **757,096,631** | **2,878,062,423** | **-** | **20,312,118,208** | **26,471,698,453** | **33** |
| SL010101 Umwagiliaji maji | 67,969,945,000 | 393,523,110 | 29,345,336 | - | - | - | 20,050,000,000 | 20,472,868,446 | 30 |
| SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo-ZARI | 3,052,200,000 | - | - | 151,849,920 | 2,116,124,330 | - | - | 2,267,974,250 | 74 |
| SL010103 Maendeleo ya huduma za kilimo | 4,233,075,000 | 1,267,062,575 | 584,755,486 | - | - | - | 73,707,456 | 1,925,525,517 | 45 |
| SL010104 Uhakika wa chakula na lishe | 1,613,072,000 | 222,152,335 | 27,582,349 | - | - | - | 188,410,752 | 438,145,436 | 27 |
| SL010105 Karakana ya Matrekta | 2,162,500,000 | - | - | 605,246,711 | 761,938,093 | - | - | 1,367,184,804 | 63 |
| | | | | | | | | | |
| **PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **5,846,648,000** | **1,516,257,850** | **83,170,794** | **-** | **-** | **-** | **-** | **1,599,428,644** | **27** |
| SL010201 Maendele ona Uhifadhi wa misitu | 5,846,648,000 | 1,516,257,850 | 83,170,794 | - | - | - | - | 1,599,428,644 | 27 |
| | | | | | | | | | |
| **PL0103 MaendeleoyaMifugo** | **3,688,990,000** | **1,087,642,180** | **59,928,494** | **179,372,000** | **604,280,425** | **-** | **-** | **1,931,223,099** | **52** |
| SL010301 Uzalishaji wa mifugo | 1,546,090,000 | 1,087,642,180 | 59,928,494 | - | - | - | - | 1,147,570,674 | 74 |
| SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo | 2,142,900,000 | - | - | 179,372,000 | 604,280,425 | - | - | 783,652,425 | 37 |
| | | | | | | | | | |
| **PL0105 Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Kilimo** | **14,267,208,000** | **3,707,797,032** | **788,987,972** | | | | **1,437,589,874** | **5,934,374,878** | **42** |
| SL010501 Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili na mifugo | 2,362,167,000 | 1,168,185,917 | 482,330,578 | - | - | - | - | 1,650,516,495 | 70 |
| SL010502 Mipango, sera na utafiti | 8,384,373,000 | 219,174,985 | 36,710,734 | - | - | - | 1,437,589,874 | 1,693,475,593 | 20 |
| SL010503 Uratibu Ofisi kuu Pemba | 3,520,668,000 | 2,320,436,130 | 269,946,660 | | | | | 2,590,382,790 | 74 |
| **JUMLA KUU** | **102,833,638,000** | **8,194,435,082** | **1,573,770,431** | **936,468,631** | **3,482,342,848** | **-** | **21,749,708,082** | **35,936,725,074** | **35** |

**Kiambatanisho Nam. 3C:**

**Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2021/2022 |
|---|---|---|
| | | |
| **OFISI KUU PEMBA** | | **293,541,000** |
| 1422022 | Ada Ya MazaoYa Misitu | 43,651,000 |
| 1421001 | MauzoYaUzalishaji Wa Miche | 1,500,000 |
| 1422060 | MapatoYa Mashamba | 196,300,000 |
| 1422048 | Ada Ukaguzi Wa Mazao | 27,710,000 |
| 1421011 | Utibabu WaWanyama | 13,780,000 |
| 1422068 | MapatoYaMifugo | 600,000 |
| 1422066 | UingizajiWaWageni Ngezi | 10,000,000 |
| **JUMLA PEMBA** | | **293,541,000** |
| | | |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | **1,048,000,000** |
| 1422022 | Ada YaMazaoYaMisitu | 250,000,000 |
| 1421001 | MauzoYaUzalishaji Wa Miche | 8,000,000 |
| 1422066 | Uingizaji Wa Wageni Jozani | 790,000,000 |
| | | |
| **IDARA YA KILIMO** | | **100,000,000** |
| 1422048 | Ada Ukaguzi Wa Mazao | 100,000,000 |
| | | |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | **120,000,000** |
| 1423002 | Mauzaji Ya Mazao Na Miche | 25,000,000 |
| 1422060 | MapatoYa Mashamba | 75,000,000 |
| 1422066 | Ada YaUingizaji Wageni | 20,000,000 |
| | | |
| **IDARA YA MIFUGO** | | **2,338,459,000** |
| 1421011 | Utibabu WaWanyama | 2,337,885,000 |
| 1422068 | MapatoYa Mifugo | 574,000 |
| | | |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | **100,000,000** |
| 1421014 | Huduma Za Matrekta | 100,000,000 |
| | | |
| **JUMLA UNGUJA** | | **3,706,459,000** |
| | | |
| **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | | **4,000,000,000** |

**Kiambatanisho Nam. 3D:**

**MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022**

| Program | Makadirio | Mshahara | Matumizi mengineyo | Ruzuku m/mengineyo | Ruzuku mshahara | Maendeleo smz | Maendeleo muhisani |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| **PL0101 Maendeleo ya Kilimo** | **37,308,868,500** | **2,861,716,553** | **2,292,293,947** | **2,072,600,000** | **3,176,500,000** | **3,020,000,000** | **23,885,758,000** |
| SL010101 Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji | 26,772,192,000 | 616,704,459 | 362,811,541 | - | - | 2,900,000,000 | 22,892,676,000 |
| SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo-ZARI | 2,895,000,000 | - | - | 560,800,000 | 2,334,200,000 | - | - |
| SL010103 Maendeleo ya Huduma za kilimo na Uhakika wa Chakula | 5,287,576,500 | 2,245,012,094 | 1,929,482,406 | | | 120,000,000 | 993,082,000 |
| SL010104 Uhakika wa chakula na lishe | - | - | - | - | - | - | |
| SL010105 Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 2,354,100,000 | - | - | 1,511,800,000 | 842,300,000 | - | - |
| | | | | | | | |
| **PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **2,766,841,500** | **2,245,646,324** | **21,195,176** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| SL010201 Maendeleo na Uhifadhi wa misitu | 2,766,841,500 | 2,245,646,324 | 21,195,176 | - | - | - | - |
| SL010202 Usimamizi wa Maliasili zisizorejesheka | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **PL0103 Maendeleo ya Mifugo** | **6,681,816,000** | **1,630,676,145** | **695,344,854** | **685,400,000** | **706,300,000** | **2,964,095,000** | **-** |
| SL010301 Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 5,290,116,000 | 1,630,676,145 | 695,344,854 | | | 2,964,095,000 | |
| SL010302 Huduma za utabibu wa mifugo | | | | | | | |
| SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo | 1,391,700,000 | - | - | 685,400,000 | 706,300,000 | - | - |
| | | | | | | | |
| **PL0105 Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Kilimo** | **6,947,227,000** | **5,890,760,978** | **1,056,466,022** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| SL010501 Utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo, Umwagiliaji maliasili na mifugo | 2,404,731,500 | 1,916,702,447 | 88,029,053 | - | - | - | - |
| SL010502 Mipango, sera na utafiti | 612,252,500 | 328,661,103 | 283,591,397 | - | - | - | - |
| SL010503 Uratibu Ofisi kuu Pemba | 3,930,243,000 | 3,645,397,428 | 284,845,572 | - | - | - | - |
| | | | | | | | |
| **JUMLA KUU** | **53,704,753,000** | **12,628,800,000** | **4,565,300,000** | **2,758,000,000** | **3,882,800,000** | **5,984,095,000** | **23,885,758,000** |

**Kiambatanisho Nam. 3E:**

**MAKADIRIO YA FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2021/2022**

